Benki ya Dunia yatoa mchongo ajira kwa vijana Tanzania ..Uk.4

Mitandao @JAMVILAHABARI Jamvi la habari jamvihabari +255676807684 Email: jamvinews@gmail.com

GAZETI LAKO

# JAMVI LA HABARI

ISSN Na 2683 - 6548: Toleo Na. 2516 IJUMAA JANUARI 31, 2024 Bei Tsh. 1000 Kenya Ksh. 60 www.jamvilahabari.co.tz

# WASSIRA: CHADEMA WATAUONA URAIS KWENYE RUNINGA TU

Uk.2







## Chadema washauriwa Kutosusia uchaguzi

NA MWANDISHI WETU

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu nchini Tanzania (LHRC), kimetoa wito kwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kujiupanga ili kiweze kushiriki Uchaguzi Mkuu wa nchi licha ya kuwa na madai ya Katiba mpya na mabadiliko kwenye mfumo wa uchaguzi hayatofanyiwa kazi na serikali.

Wito huo wa LHRC unafuatia msimamo ulio-

>> Inaendelea Uk.4

## Dkt. Samia aahidi serikali kukabiliana na maafa nchini



Uk.3

# DKT SAMIA AAHIDI SERIKALI KUKABILIANA NA MAAFA NCHINI

NA MWANDISHI WETU

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema Serikali itaimarisha mifumo ya usimamizi wa maafa na kuhakikisha inakuwa na utayari wa kukabiliana na dharura wakati wote. Dkt. Samia aliyasema hayo jana katika hafla ya chakula cha mchana pamoja na washiriki wa zoezi la utafutaji na uokozi wa ajali ya kuporomoka kwa jengo la ghorofa eneo la Kariakoo, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi aliyoitoa wakati alipotembelea eneo la ajali mwezi Novemba, 2024.

Aidha Rais Dkt. Samia ametumia hafla hiyo kuwashukuru wote waliojitolea katika zoezi la utafutaji na uokozi na amerejea msisitizo wake kuwa taarifa ya Kamati ya

Uchunguzi wa ajali ya jengo kuporomoka Kariakoo, itakapokamilika itawekwa wazi.

Kwa upande mwingine, Rais Dkt. Samia ameridhia mwaliko wa Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Kariakoo kufanya ziara katika eneo hilo la biashara kwa lengo la kuzungumza na wafanyabiashara wa eneo hilo.

Akijibu mwaliko kutembelea Kariakoo, Rais Dkt. Samia alisema atatumia ziara hiyo pia kuzindua ukarabati wa jengo la Soko Kuu la Kariakoo huku akirejea azma ya Serikali kulifanya soko la Kariakoo kufanya biashara kwa saa 24.



# CHADEMA WASHAURIWA KUTOSUSIA UCHAGUZI

NA MWANDISHI WETU

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu nchini Tanzania (LHRC), kimetoa wito kwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kujiupanga ili kiweze kushiriki Uchaguzi Mkuu wa nchi licha ya kuwa na madai ya Katiba mpya na mabadiliko kwenye mfumo wa uchaguzi hayatofanyiwa kazi na serikali

Wito huo wa LHRC unafuatia msimamo uliotangazwa na mwenyekiti mpya wa CHADEMA Tundu Antipas Lissu kuwa chama hicho hakitoshiriki kwenye uchaguzi huo wa mwezi oktoba kama matakwa yao yatapuuzwa.

Hata hivyo licha ya kauli ya Mwenyekiti wa chama hicho Tundu Lissu lakini katika hutoba yake aliyoitoa juzi wakati akikaribishwa Makao makuu ya chama hicho, Mikocheni Jijini Dar es salaam alikaririwa akiwataka Wanachadema waliokuwa nje warejee ili kujipoanga vizuri kuelekea uchaguzi huo.

# BENKI YA DUNIA YATOA MCHONGO AJIRA KWA VIJANA TANZANIA

NA MWANDISHI WETU

RAIS wa Benki ya Dunia (WB) Ajay Banga ametoa matumaini kwa vijana wa Kiafrika wakiwemo Watanzania, kujiandaa kuingia kasika soko la ajira ikiwa ni sehemu ya mipango inayoendelea kukamilika ya taasisi hiyo.

Alisema katika muongo ujao, Vijana milioni 360 wa Afrika watakuwa tayari kuingia kwenye soko la ajira, kipindi ambacho pia mfumo wa Afrika unatarajiwa kutoa ajira kwa vijana milioni 250.

Banga aliyasema hayo hii leo Januari 28, 2025 katika Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika ulioingia katika siku yake ya pili jijini Dar es Salaam na kuongeza kuwa kipindi hicho pia kitawaacha vijana watatu kati ya watano, bila fursa ya kazi inayowapa kipato na heshima.

Amesema ili Afrika ifaidike, sote tunahitaji kubadili mtazamo huu, kwa sababu makadirio si hatima. Tunaweza kubadili hali hii na kuwasaidia hao vijana watatu kati ya watano.

Rais huyo wa WB pia amesema safari za mafanikio zinaendeshwa kwa matumaini, lakini uhalisia unatimizwa kwa vitendo.

# ASSIRA AISHIKA PABAYA CHADEMA

NA MWANDISHI WETU, GEITA

ZIARA ya Makamu Mwenyekiti wa CCM Mzee Steven Wassira mjini geita kwa kiasi kikubwa imebomoa ngome ya Chama Cha Demokrasia na Maendeleo Chadema, baada ya hotuba ya kiongozi huyo kufichua mapungufu makubwa katika chama hicho cha siasa.

Mzee Wassira aliwasili mkoani Geita kwa ziara ya kikazi ambapo pamoja na mambo mengine alizindua sherehe za maadhimisho ya miaka 48 ya kuzaliwa CCM kwa Mkoa wa Geita.

Baada ya kuwasili mkoani humo na kulakiwa na viongozi wa Chama wa mkoa huo pamoja na serikali wakiongozwa na Mkuu aa Mkoa wa Geita, kisha kupokea taarifa ya Chama na utekelezaji wa Ilani ya CCM katika kikao kilichofanyika ofifisi za CCM za mkoa huo.

Baadaye alipata nafasi ya kuzungumza na mamia ya wananchi wa geita ambapo aliwaeleza jinsi chama hicho cha upinzani kilivyojaa 'Machawa' hususan Makamu mwenyekiti wa chama hicho John Heche ambaye amemtaja kuwa hana hata siufa moja ya kuwa kiongozi wa chama cha siasa.

Aidha makamu huyo wa CCM amewataka Wananchi wa Geita kuendelea kumuunga mkono bila kusikiliza kelele za wapinzani kwa vile yeye bado ana uwezo wa kukiongoza chama licha ya umri wake mkubwa.

Awali Makamu mwenyekiti wa Chadema John alitoa maneno ya kejeli akidai kuwa Mazee wassira hawezi kushindana na Mwenyekiti wao Tundu Lisu kwa vile amefanya kazi zaidi ya miaka 60, kauli ambayo imejibiwa na Makamu huyo Mwenyekiti wa CCM akisema kwamba licha ya umri wake lakini abado ana mawazo ya kisasa na anayetambua umuhimu wa CCM kuendelea kushika dola.

Katika mkutano huo wakazi wa geita walieleza matumaini yao makubwa kwa Mwenyekiti wa Chama hicho ambaye poia ni rais wa Tanzania Dkt samia Suluhu hassan kutokana na juhidi anazofanya kuboresha maisha ya wananchi.

Naye Mbunge wa Geita Mjini Joseph Msukuma alisema kuwa CCM katika uchaguzi ujao itafanya kampeni zake kwa kuonyesha maendeleo iliyopata ambayo mni kjuhidi kubwa za rais Dkt Samia pamoja na viongozi waliotokana na Chama Cha Mapinduzi ambao wameendelea kuteleza Ilani ya Chama na kuwaletea maendeleo wananchi wake.

# KITUO CHA KIBANGA KUTOA HUDUMA SAA 24

NA. PETER HAULE, WF, DODOMA

SERIKALI imesema kuwa inafanya jitihada ili Kituo cha Forodha cha Pamoja (OSBP) Kabanga, kinachotoa huduma kati ya Tanzania na Burundi, kiweze kutoa huduma saa 24 ili kuongeza ufanisi.

Hayo yameelezwa bungeni jijini Dodoma na Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Ngara, Mhe. Ndaisaba George Ruhoho, aliyetaka kujua mkakati wa Serikali wa kuwezesha Vituo vya Forodha vya Murusagamba na Kabanga, kufanya kazi saa 24.

Mhe. Chande alisema kuwa Kituo cha Forodha cha Kabanga ni Kituo cha Pamoja (OSBP) cha kutoa huduma za forodha kati ya Tanzania na Burundi ambacho kina miundombinu wezeshi kama vile taa za ulinzi, vyombo vya ulinzi na usalama, na maeneo ya kukagulia bidhaa, wasafiri na wafanyakazi, hivyo kuwa na uwezo wa kufanya kazi saa 24 kwa upande wa Tanzania.

"Ili Kituo hicho kiweze kutoa huduma saa 24, upande wa Kobero nchini Burundi unapaswa pia kuwa tayari kutoa huduma hizo saa 24", alieleza Mhe. Chande.

Alisema kuwa kwa sasa Kituo cha OSBP Kobero kwa upande wa Burundi kinatoa huduma kwa saa 12 tu, hivyo jitihada mbalimbali zinaendelea kufanyika ili kuwezesha mazingira ya Kituo cha OSBP Kobero kufanya kazi saa 24, hususan ulinzi na usalama.

Akieleza kuhusu Kituo cha Murusagamba, Mhe. Chande alisema kuwa Kituo hicho ni kidogo cha forodha kinachofanya kazi ya uzuiaji (Preventive office), ambapo hufanya kazi ya kuzuia magendo kwenye maeneo ambayo mwenendo wa bidhaa na watu ni mdogo.

Naibu Waziri Mhe. Chande alisema kuwa, kutokana na udogo wa mwenendo wa bidhaa na watu katika Kituo cha Murusagamba uwezekano wa kituo hiki kufanya kazi saa 24 kwa sasa haupo.

Akijibu maswali ya nyongeza kuhusu ufungaji wa kifaa cha ukaguzi (Scaner) eneo la Mtukula lililopo mpaka wa Tanzania na Uganda na Kituo cha Horohoro Tanga kati ya Tanzania na Kenya, Mhe. Chande alisema kwa upande wa Mtukula, tayari Mkandarasi yupo eneo la mradi kwa ajili ya kufunga kifaa hicho na upande wa Horohoro, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inaangalia utekelezaji wake.

Kwa upande mwingine alisema mazungumzo yanaendelea kuhusu uwezekano wa Kituo cha Forodha cha Malindi kilichopo Zanzibar kiweze kufanya kazi saa 24 kwa kuwa kwa sasa kinahudumia Kontena 2,000 kwa mwezi licha ya kufanyakazi kwa saa 12.

Alisema kuwa wanaendelea na mazungumzo na upande wa Zanzibar, ambapo kukamilika kwa mazungumzo hayo kutawezesha huduma hiyo.

# WASSIRA AISHIKA PABAYA CHADEMA

NA MWANDISHI WETU, GEITA

ZIARA ya Makamu Mwenyekiti wa CCM Mzee Steven Wassira mjini geita kwa kiasi kikubwa imebomoa ngome ya Chama Cha Demokrasia na Maendeleo Chadema, baada ya hotuba ya kiongozi huyo kufichua mapungufu makubwa katika chama hicho cha siasa.

Mzee Wassira aliwasili mkoani Geita kwa ziara ya kikazi ambapo pamoja na mambo mengine alizindua sherehe za maadhimisho ya miaka 48 ya kuzaliwa CCM kwa Mkoa wa Geita.

Baada ya kuwasili mkoani humo na kulakiwa na viongozi wa Chama wa mkoa huo pamoja na serikali wakiongozwa na Mkuu aa Mkoa wa Geita, kisha kupokea taarifa ya Chama na utekelezaji wa Ilani ya CCM katika kikao kilichofanyika ofifisi za CCM za mkoa huo.



Baadaye alipata nafasi ya kuzungumza na mamia ya wananchi wa geita ambapo aliwaeleza jinsi chama hicho cha upinzani kilivyojaa 'Machawa' hususan Makamu mwenyekiti wa chama hicho John Heche ambaye amemtaja kuwa hana hata siufa moja ya kuwa kiongozi wa chama cha siasa.

Aidha Makamu huyo wa CCM amewataka Wananchi wa Geita kuendelea kumuunga mkono bila kusikiliza kelele za wapinzani kwa vile yeye bado ana uwezo wa kukiongoza chama licha ya umri wake mkubwa.

Awali Makamu mwenyekiti wa Chadema John alitoa maneno ya kejeli akidai kuwa Mzee wassira hawezi kushindana na Mwenyekiti wao Tundu Lisu kwa vile amefanya kazi zaidi ya miaka 60, kauli ambayo imejibiwa na Makamu huyo Mwenyekiti wa CCM akisema kwamba licha ya umri wake lakini bado ana mawazo ya kisasa na anayetambua umuhimu wa CCM kuendelea kushika dola.

Katika mkutano huo wakazi wa geita walieleza matumaini yao makubwa kwa Mwenyekiti wa Chama hicho ambaye poia ni rais wa Tanzania Dkt samia Suluhu hassan kutokana na juhudi anazofanya kuboresha maisha ya wananchi.

Naye Mbunge wa Geita Mjini Joseph Msukuma alisema,kuwa CCM katika uchaguzi ujao itafanya kampeni zake kwa kuonyesha maendeleo iliyopata ambayo ambayo ni kazi kubwa iliyofanywa na Rais Samia pamoja na viongozi waliotokana na Chama Cha Mapinduzi ambao wameendelea kuteleza Ilani ya Chama na kuwaletea maendeleo wananchi wake.

# Uchaguzi Chadema umeacha mpasuko mkubwa

NA MWANDISHI WETU




TANGU ulipofanyika uchaguzi Mkuu wa Chama cha Siasa cha upinzani (Chadema), kumekuwa na mitazamo mingi inayozungumzia hali illiyo na itakavyokuwa ndani ya chama lakini, wadadisi wengi wanaona mapunhgufu makubwa yaliyojitokeza.

Chama hicho mpaka sasa ni kama vile kimesjhampoteza Mwanasiasa mashuhuri Freeman Mbowe ambaye licha ya kutamka hadharani kwamba ataendelea kuwa mtitifu na mshauri wa chama hicho lakini ni kama vile ameshajiuweka pembeni.

Hii inatokana na ukweli kwamba Mwenyekiti huyo aliyedumu kwa zaidi ya miongo miwili akikiongoza chama hicho tangu alipopokea kijiti kutoka kwa Mzee Bob Makani zaidi ya miaka 20 iliyopita, hawezi kufanya kazi pamoja na Mwenyekikiti wa sasa Tundu Lissu amnbaye alijitokeza hadharani na kumkashifu kwa masuala mbalimbali ikiwemo tuhuma za kukihujumu chama.

Kauli ya Mbowe kuonyesha mshikamano hata baada ya kubwagwa ilionekana kama ni kauli za kisiasa tu kwa vile hata siku aliyotarajiwa kwenda kumkabishi ofisi Mwenyekiti huyo yeye hakuonekana katika sherehe hizo zilizofanyika juzi Makao Makuu ya Chama hicho Mikocheze.

Ukiacha wadau mbali mbali wa kisiasa wanaoonyesha hofu yao juu ya usalama wa Chadema na hasa kujenga mshikamano kama wanaounadi ni pamoja na kiongozo wa Jumuia ya Wazazi ya CCM

Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) imekibeza Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), ikidai kuwa uchaguzi wa viongozi wake wa juu umewaachia vidonda, majereha na makovu yasiyoisha, hivyo haina shaka kuwa CCM itashinda kwa kishindo katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Hivi karibuni, CHADEMA ilifanya uchaguzi wake wa ndani ambapo Tundu Lissu alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa chama hicho, akimshinda Freeman Mbowe, ambaye amekiongoza chama hicho kwa zaidi ya miaka 20.

Akizungumza Jijini Dodoma, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi wa CM, Fadhili Maganya, pamoja na Katibu Mkuu wake, Ally Hapi, wamesema CCM tayari imepata wagombea wake na inaendelea kujiandaa na uchaguzi, tofauti na CHADEMA ambayo bado inatibu majeraha ya uchaguzi wake wa ndani.




"Tayari tumepata mgombea wetu, tumejiandaa na uchaguzi. Wao wamemaliza uchaguzi na sasa wanatibu vidonda na majereha. Hakuna sehemu imetulia kama CCM kwa sasa," amesema Maganya.

Katika hatua nyingine, Maganya ametangaza kuwa Jumuiya ya Wazazi itaandaa kongamano maalumu Februari 2, 2025, kuelekea sherehe za miaka 48 ya CCM, zitakazofanyika Februari 5 jijini Dodoma.

Amesema kongamano hilo litashirikisha wadau mbalimbali, ambapo mada muhimu zitajadiliwa, zikiwemo mchango wa CCM katika maendeleo ya taifa, nafasi ya Dk. Samia Suluhu Hassan katika ujenzi wa chama, na umuhimu wa vijana na elimu katika maendeleo.

Maganya amesisitiza kuwa kuelekea miaka 48 ya CCM, chama hicho kina kila sababu ya kujivunia mafanikio yake, ikiwemo amani na maendeleo yanayoonekana nchini.

# MAENDELEO MAKUBWA YA TEKNOLOJIA YANAKUJA MNH

NA MWANDISHI WETU

WIRARA ya Afya inaendelea kupiga hatua katika masuala ya teknolojia, ukiwa ni mkakati wa serikali kuhakikisha Tanzania inapiha hatua katika kutoa tiba za kibingwa na kuwa na uwezo wa kutosha kukabiliana na maradhi ya aina yoyote na kuyapatia ufumbuzi ndani ya nchi.

Hivi karibuni Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi, amesema hospitali hiyo, inatarajia kuja na kifaa cha kisasa cha kupima ugonjwa wa kisukari kwa njia ya mate.

Amesema kutokana na kukua kwa matumzi ya vifaatiba vya kiteknolojia duniani, hospitali hiyo yenye hadhi ya kitaifa na kimataifa ni matarajio kuwa na aina tofauti za utaalamu wa hali ya juu na kisasa.

Prof. Janabi, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, muda mfupi baada ya MNH kukabidhiwa vifaatiba mbalimbali, vyenye thamani ya Sh. milioni 125, ikiwamo maalumu kwa ajili ya kukuza uoni wa mishipa ya damu na fahamu wakati wa upasuaji.




Vifaa hivyo vilikabidhiwa na Balozi wa China nchini, Chen Mingjian, kwa Waziri wa Afya, Jenista Mhagama, hospitalini hapo, kwa niaba ya Serikali ya Watu wa China, jijini Dar es Salaam.

"Tutakapokuwa tayari tututaarifu umma kupitia nyinyi waandishi wa hbari. Tutakuwa na kifaa kipya cha kupima kisukari kwa njia ya mate," alisema Prof. Janabi.

Kwa mujibu wa wataalamu wa afya, ugonjwa wa kisukari ni ugonjwa sugu ambao mtu yeyote anaweza kuugua. Inakadiriwa kuwa watu milioni 422 wanaishi na ugonjwa wa kisukari duniani kote, ikiwa ni mara nne zaidi ya miaka 40 iliyopita, kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

Ugonjwa wa kisukari hutokea wakati mwili hauwezi kutumia sukari inayotengenezwa na mwili (glucose) yote katika damu.

Kwa kawaida glucose yenyewe si mbaya, kwani nimafuta ya seli zote katika mwili kwa baadhi ya tishu, kutumia glucose hiyo, zinahitaji hatua ya insulini, ambazo ni homoni zinazozalishwa na kongosho ambayo inaruhusu sukari hiyo kupenya kwa urahisi zaidi ndani ya seli na hivyo kubadilishwa kuwa nishati.

Matatizo ya kisukari yanaweza kusababisha mshtuko wa moyo, kiharusi, upofu, kushindwa kufanya kazi kwa figo na kukatwa kwa viungo vya mwili.

Licha ya hatari, watu wengi wenye ugonjwa wa kisukari hawajui kuwa wanao. Mabadiliko ya mtindo wa maisha yanaweza kuzuia mtu kuugua kisukari.


# TANGAZA NASI SASA

*Unatamani kukuza biashara yako kutoka hapo ilipo kuwa kubwa na yenye mantiki zaidi?*

- *Unatamani kuongeza kipato, uelewa na upana wa shughuli zako za kila siku?*
- *Je unataka kuwafikia wateja wako ndani na nje ya nchi kwa kiasi kikubwa ili kukuza biashara na huduma yako?*
- *Fahamu kwamba JAMVI LA HABARI na mitandao yake ya kijamii kama Youtube, Instagram, Facebook, Website na Twitter hutembelewa na maelfu ya wasomaji kila siku Duniani kote.*
- *Hivi unafahamu kuwa JAMVILAHABARI kwa sasa ni moja kati ya Media chache zinazo ongoza kwa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati zinazotokea nchini na Duniani kwa ujumla?*

*TANGAZA SASA NA JAMVI LA HABARI KWA PUNGUZO KUBWA LA BEI UPATE MATOKEO YA HARAKA.*

*Kwa matangazo yote kama vile minada, kupotelewa kwa vyeti vya shule, matangazo ya makampuni, nafasi za kazi, zabuni za kazi, maonyesho, dawa za asili, taasisi za elimu, taasisi za dini na mengine mbalimbali mbali mbali.*

*Ni rahisi sana, wasiliana nasi kupitia Whatsap namba +255659555744 au tupigie katika +255743777778 au +255659555744 GHARAMA ZETU NISAWA NA BUREE JAMVILAHABARI; TUMECHAGUA KUKUHUDUMIA www.jamvilahabari.co.tz*

# MAMLAKA YA HALI NA UMAKINI KUTOA TAHADHALI



NA MWANDISHI WETU

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imesema mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa kunyesha katika maeneo mengi ya Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki pamoja na Mashariki mwa mikoa ya Mara na Simiyu.

Mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zikitarajiwa katika maeneo ya Pwani ya Kaskazini, Kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma na Ukanda wa Ziwa Victoria.

Akizungumza Jijini Dar es Salaam wakati akitoa utabiri wa mwelekeo wa mvua za masika 2025 Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA, na Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi, Dkt. Ladislaus Chang'a amesema kuwa mvua hizo zinatarajiwa kuanza wiki ya Pili au ya tatu ya mwezi Machi mwaka huu.

Amesema mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo ya Pwani ya Kaskazini, Kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma na Ukanda wa Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga na magharibi mwa mikoa ya Simiyu na Mara) katika kipindi cha Msimu wa Masika, 2025.

Amesema mwelekeo wa mvua za masika 2025 kwa Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu na Mara) pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma, mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani zitaanza wiki ya kwanza hadi ya pili ya mwezi Machi na kuisha wiki ya kwanza ya mwezi Mei.

Aidha mikoa ya Pwani ya Kaskazini (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Tanga na visiwa vya Unguja na Pemba) inatarajiwa kuwa na mvua za wastani hadi chini ya wastani ambazo zitaanza wiki ya kwanza hadi ya pili ya mwezi Machi na kumalizika wiki ya tatu hadi ya nne ya mwezi Mei.

Pia Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), inatarajiwa kuwa na mvua za wastani hadi juu ya wastani ambapo zitaanza wiki ya pili hadi ya tatu ya mwezi Machi na kumalizika wiki ya kwanza mwezi Mei.

Ameongeza kuwa ongezeko la mvua hizo zinatarajiwa katika kipindi cha mwezi Aprili sambamba na kutoa angalizo la matukio ya hali mbaya ya hewa ikiwemo vipindi vya mvua kubwa kujitokeza hata katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani.

Pia, Dkt. Chang'a ametaja athari zinazoweza kujitokeza katika Mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani kuwa kupelekea upungufu wa upatikanaji wa maji katika baadhi ya maeneo hasa matumizi ya majumbani, kilimo na ufugaji.

"Vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri ukuaji wa mazao katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani, wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea yanayoendana na hali ya ongezeko la unyevu kama vile ukungu yanatarajiwa kuongezeka na kuathiri mazao kama ndizi, mahindi, mpunga, mihogo na maharage," amesema.

Aidha amewashauri wakulima kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa kuzingatia hali ya unyevu katika udongo, kutumia mbinu bora na teknolojia za kuzuia maji kutuama shambani, kuhifadhi maji shambani, kuzuia mmomonyoko na upotevu wa rutuba kutokana na kutuwamisha maji kwa muda mrefu au mafuriko.

"Wakulima wanashauriwa kutafuta taarifa sahihi kutoka kwa maafisa ugani kwa kuzingatia utabiri wa msimu wa wilaya husika katika kuchagua mbegu na zao sahihi." amesisitiza.

Amewashauri wakulima na maafisa ugani kuendelea kutumia utabiri wa kila siku na siku kumi ili kufuatilia kwa ukaribu mwenendo wa utabiri wa msimu.

# TAHARIRI

## Hongera Dkt. Samia kwa kuwafariji wahanga Kariakoo

JANA Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,Dkt. Samia Suluhu Hassan aliwapa matumaini Watanzania akisema Serikali itaimarisha mifumo ya usimamizi wa maafa na kuhakikisha inakua na utayari wa kukabiliana na dharura wakati wote.

Aliyazungumza hayo katika hafla ya chakula cha mchana pamoja na washiriki wa zoezi la utafutaji na uokozi wa ajali ya kuporomoka kwa jengo la ghorofa eneo la Kariakoo, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi aliyoitoa wakati alipotembelea eneo la

ajali mwezi Novemba, 2024.

Katika hafla hiyo pia Dkt aliyefuatana na waziri Mkuu majaliwa Kassim majali, ali washukuru wote waliojitolea katikazoezi la utafutaji na uokozi na amerejea msisitizo wake kuwa taarifa ya Kamati ya

Uchunguzi wa ajali ya jengo kuporomoka Kariakoo, itakapokamilika itawekwa wazi.

Sisi Jamvi la habari tunatoa pongezi wa Serikali hususan Rais Dkt Samia kwa kuonyeshwa kuguswa kwake na tukio lile lililochukua uhai wa watanzania kadhaa na wengine kujeruhiwa.

Aidha tunapata faraja kufuatia mikakati ya serikali juu ya kuimarisha mifumo ya ukozi wa majanga kwa muda mfupi, tunaamini hili litasaidia kuoakoa hali na maloi za jamii endapo yataokea matukio mengine ya aina ile.

Pamoja na kushukuru juhudi hizo za seikali pia tunawashauri wananchi kuongeza umakini wanapotumia majengo hasa ya ghorofa kuhakikisha kuwa usalama unatamalaki, ili kuepuka na matukio yoyote ya hatari yanapotokea basi yasigharimu maisha ya watu wengi kama ilivyokuwa Kariakoo.

Tunaziomba pia mamlaka zinahusika na ukaguzi wa majengo kuhakikisha hawalali usiku na mchana kwa vile kasi inayoonekana hivi sasa katika miji mikuu, ina kila dalili ya kuhusisha wajenzi wasiokidhi vigezo ambao wanaweza kusababisha ajali za aina ile.

BODI YA UHARIRI

Mhariri Mkuu - 0762 178 678
Idara Ya Matangazo/Masoko - 0743 777 778,
- 0659 555 744
Idara Ya Usambazaji - 0676807684,
- 0787 288 160

Gazeti hili hutolewa na **JAMVI MEDIA GROUP**
S. L. P 78862, Dar es Salaam
**Tel:** +255 676 807684, 255 743 777778
**Email:** jamvinews@gmail.com
www.jamvilahabari.co.tz



*Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), Mhandisi Victor Seff, akikagua mradi wa barabara za Mtili – Ifwagi (Km. 14) na Wenda – Mgama (Km. 19) ambazo zinagharimu Shilingi Bilioni 52 mkoani Iringa, jana.*

UCHAMBUZI

# Uahindi wa CCM unatokana na utekelezaji wa ilani yake

NA MWANDISHI WETU

SIRI kubwa ya maandalizi ya CCM Kushinda uchaguzi Mkuu na kuendelea kushika Doila, ni utekelezaji wa Ilani ya chama hicho ambayo viongozi, waliopewa nafasi waliibeba na kuifanyia kazi kila eneo.

Hilo ndilo linaloweza kuwafanya wagombea wa chama hicho akiwemo mgombea nafasi ya Urais Dkt Samia Suluhu Hassan pamoja na jopo la wviongozi wengine watakaopambania nafasi za Ubunge na Madiwani.

Tayari chama hicho kimefanya chaguzi za ndani kama vile ule uliohusisha Mkutano Mkuu wa CCM, ulimchagua Mzee Steven wassira kuwa Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Bara.

Wassura aliyekuwa nje ya madaraka ya kisiasa kwa muda mrefu kwa maneno yake mwenyewe alieleza kushangazwa na ushindi ule na akaahidi kuifanya kazi hiyo kwa uadilifu na unyenyekevu mkubwa, kama hatua ya kulipa fadhjila na heshima ile kubwa.

Pia mkongwe huyo akatabiri ushindi wa kishindo utakaokipata chama chake, mtaji mkubwa ukiwa ni utekelezaji wa Ilani na jinsi chama hicho kinavyoendesha siasa zake kwa njia ya uwazi na uwajibikaji.

Mkongwe huyo ameingia na Falsafa ya Umoja Maridhiano na Ushindi, kazi ambayo amewaahidi wajumbe waliomuamini kushika wadhifa huo kuwa ataifanya kwa bidii kubwa huku akiamini ni jukumu lenye baraka za Mungu.

Kwa tathmini nyepesi ya ushindi huu wa Wasira una maana kubwa kwa CCM kuekelea uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika mwaka huu, mwezi Okttoba kwamba mtaji wake unaonekana umeongezeka

Ukichukulia kuwa CCM ndicho chama kinachoongoza nchini kwa kuwa na wanachama na wapenzi wengi kinaweza kutumia mtaji huo kumpa ushindi wa kishindo mgombea wake wa Urais na hata Wabunge na Madiwani.

CCM ina watu wengi hata isipohitaji kura ya wapinzani au watu wasiofungamana na siasa ya chama chochote bado wana uhakika wa kushinda hususa nafasi ya Urais pengine baadhi ya wabunge wachache wanaweza kupoteza viti kutokana na kutowafanyia vizuri wapiga kura wao katika kipindi kilichopita.

Mgombea wa CCM anasaidiwa na maendeleo yanayoonekana kila kona, atahitaji timu ya kawaida tu kumnadi na kuweza kumpa ushindi wa kimbunga kama huu alioanza kuonyesha dalili Mzee Wasira

Ushindi wa CCM mwaka huu unaonekana bila kuhitaji utafiti mkubwa, kwani hata ukiangalia upande wa upinzani bado unaonekana kama hakuna chama chenye nguvu kama ilivyokuwa katika chaguzi za awamu zilizoipita tangu kuanzishwa mfumo wa vyama vingi vya Siasa mwaka 1992

Licha ya CCM kujiandaa kama ilivyokuwa wakati wote inapoingia katika uchaguzi, lakini mwaka huu licha ya uwepo wa maridhiano ya kisiasa, lakini upinzani unaonekana kupoteza nguvu kuliko miaka yote ya uchaguzi.

Ni mwaka tutakaoendelea kusikia vishindo vya CCM katika majimbo na makelele ya wapinzani watakaoendeleza msamiati wa kuibiwa kura ili hali hawakuwa na maandalizi zaidi ya malumbano na kukashifiana.

# Ukatili wa kijinsia uko

NA OSCAR ASSENGA, TANGA



ASKOFU wa Jimbo Katoliki la Tanga Mhashamu Thomas Kiangio ametaka hatua kali zichukuliwe kwa wanaohusika na kufanya vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto ili kukomesha tabia hiyo kwenye jamii.

Aliyasema hayo wakati wa Ufunguzi wa Jubilei Kuu 2025 kwa waandishi wa Habari Jimbo Katoliki la Tanga ambapo alisema kwamba vyombo vya habari havipaswi kukaa kimya badala yake wawe mstari wa mbele kuwafichua wanaofanya vitendo hivyo.

Mhashamu Kiangio alisema kwa sababu pale ambapo vyombo bua habari vinapokaa kimya uovu unapotendeka watakuwa hawana maana yoyote ya uwepo wao kutokana na kusambaza taarifa nzuri kuacha mabaya yatendeka.

"Ukiangalie leo hii watoto wadogo wanahujumiwa wanaingizwa kwenye mifuko ya rambo vyombo vipo wapi na je wanatoa taarifa watoto wanatendwa ukatili wanauwawa wasiokuwa na hatia "alisema

Hata hivyo alisema kwamba wakati mwengine unasikia watoto wamepakiwa kwenye basi wanasafirishwa kuelekea mahali fulani wengine wapo hai wengine wamekufa lakini hawaona hatua wanayotenda kwa watu hao hivyo kuna umuhimu hatua kuchukuliwa.

"Wakati mwengine wanahabari wanatuletea taarifa za uchungu lakini hamtuambii aliyefanya hivyo ni nani na hatua gani zimechukuliwa kuweza kudhibiti vitendo vya namna hiyo kuendelea kwenye jamii"Alisema

Aidha alisema suala hilo lazima wao kama wanahabari walitafakari hasa ikiwa ni hija ya wanahabari kwamba wale ambao wanawatendea mabaya ya kuwaua watu wasiokuwa na hatia wafichuliwa na watoa taarifa kamili na wasitoe nusu nusu ili kuwezesha kukomesha vitendo hivyo

"Wana habari mnakazi kubwa sana na ndio maana Baba Mtakatifu akaifanya siku ya leo duniani ya wana habari kutokana na umuhimu wenu hivyo msiwe waongo mtoe taarifa watuhumiwa wajulikane"Alisema

Hata hivyo alisema katika suala la ukatili wa watoto Tanga ni ya pili hivyo ni wakati wa wanahabari kubadilika na kuacha kuandika nzuri badaa yake mfichue kwa umakini jambo hilo ili lisiwepo kwenye jamii.

"Salini mkimuomba mwenyezi Mungu awaongoze na kutafuta na kuona maana nyie ni kioo cha jamii lakini tuziombee familia za wana habari wengi wamepoteza maisha kutokana na kuwa wakweli kwa ndio maana wengine wanajificha"Alisema

Dawa za Kulevya.

Askofu Mhashamu Kiangio alisema Tanga inakumbwa na vijana kuingia kwenye dawa za kulevya jambo ambalo linachangia kupoteza nguvu kazi ya Taifa kutokana na kugeuka kuwa tegemezi kwenye familia zao .

"Unapotembea katika maeneo ya Bombo ukipita hapo vijana wenye afya na nguvu wameingia kwenye dawa za kulevya wanaenda kupata tiba hapo serikali inatambua lakini wale wanaowapa wafikie hivyo ni wakina nani? Alihoji Askofu Mhashamu Kiangio.

Askofu huyo alisema kwa sababu wale wanaotumia dawa za kulevya ni ndugu ,kaka na dada zenu hivyo wanahitaji watetezi ambao watawatoa kwenye janga hilo.

Hata hivyo alisema kuna hatari Taifa likaangamia kwa kutokujali wale wanaongaika pale wazazi wao wanafanya nini au ni kuwaacha kupata dawa na kurudi na kumuomba mwenyezi mungu kukomesha matumzi ya dawa za kulevya .

"Fikiria kama ni kaka yal
baba yako, ndugu yako hav
zi kupendezwa na jambo h
hivyo tuwaombee kwenye h
hii mtambua ya kweli msizus
ie watu huongo"Alisema

Jubilee hii ya mwaka 20
ina beba ujumbe bila Uchum
Sugu inawezekana jubilee
asema watu wasiishi uchum
sugu ina mana yake kwa wa
ambao hawajafunga ndoa.

Aliongeza kwamba kati
Jubilei hii ya mwaka 2025 vi
viashiria ambavyo ni msala
ulipo mbele alama ya ukomb

# omeshwe kwa kila njia



> Fikiria kama ni kaka yako, baba yako, ndugu yako hawezi kupendezwa na jambo hilo hivyo tuwaombee kwenye hija hii mtambua ya kweli msizushie watu huongo”





ko,
we-
ilo
ija
sh-

025
ba
in-
ba
ale

ka
po
ba
o-

zi na kwa kipindi cha miaka 25 ya Jubilee imeona mambo mengi yalitokea mambo makubwa kama vita ya dunia wengi walipoteza maisha.

Alisema pia magonjwa mbalimbali ya kila siku na milipuko na miaka ya karibuni kulitokea ugonjwa wa corona na watu wengi walipoteza maisha na hata sasa kumeweka moto huko Jimbo la Califonia Marekani na katika mawimbi hayo ikaonekana inafaa na kumpendeza Mungu Jubilee ya 2025 ya mahujaji katika matumaini.

# MBUNGE ASHITUKIA WANAONYEMELEA JIMBO LAKE



NA MWANDISHI WETU

MBUNGE wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki (CCM) Mkoani Morogoro, Hamis Shabani Taletale maarufu Babu Tale, amesema wenye nia ya kugombea jimbo hilo katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, waanze kujindaa kisaikolojia

Amesema wajiandae kufiLisika, kwa kuwa yeye amejipanga vyema kupambana nao kwa gharama yoyote na haogopi kutumia pesa, kwa ajili ya wananchi kupata maendeleo.

Babu Tale, amesema hayo wakati akiongea kwenye uzinduzi wa maadhimisho ya miaka 48 ya kuzaliwa kwa Chama cha Mapinduzi (CCM) yaliyofanyika kimkoa katika Tarafa ya Ngerengere iliyopo Halmashauri ya wilaya ya Morogoro mkoni humo.

Amesema kuwa alipochaguliwa kuwa mbunge wa jimbo hilo, alikuta halina maendeleo yoyote, ikiwamo ubovu wa miundombinu mbalimbali, kama vile barabara, kero sugu ya ukosefu wa maji na umeme, uhaba wa vituo vya afya na magari ya wagonjwa na upungufu wa shule za sekondari.

Amesema katika kipindi chake cha muda mfupi, ameweza kupambana na kumshawishi Rais Samia Suluhu Hassan, kutoa fedha za utekezaji wa miradi ikiwamo, ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami Bigwa-Kisaki, Ubena–Ngerengere pamoja na kufungua mitaa na vitongoji ambavyo vilikuwa havipitiki.

"Lilikuwa jimbo la mwisho kimaendeleo nikaamua kupambana, ili kuleta maendeleo ikiwamo kutumia fedha zangu za mfukoni na limepata maendeleo na kuna watu wanaumimi sana.

Sasa nasema wazi wanaokuja kugombea wanapaswa kujipanga kikamilifu na watambue watafirisika kwa kuwa nimejipanga haswa na siogopi kutumia fedha, kwa ajili ya kusaidia wananchi waendelee kupata maendeleo," amesema Babu Tale.

Ametaja changamoto nyingine aliyoitatua ni pamoja na kuchangia ujenzi wa zahanati kwenye vijiji na vituo vya afya na kutoa magari matatu ya kubeba wagonjwa katika vituo vya Ngerengere, Mkuyuni na Mikese.

"Leo natamba hapa Ngerengere mbele ya wananchi kwa kuwa nimeleta barabara ya lami kutoka Ubena-Ngerengere, nimeleta mradi mkubwa wa maji wa kutatua kero ya maji ya vijiji vitano, nimeleta gari la wagonjwa na nimesaidia ujenzi wa shule za sekondari tatu," amesema mbunge huyo.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa (MNEC) wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kupitia Mkoa wa Morogoro, Jonas Nkya, amempongeza Babu Tale, kwa kulipambania jimbo hilo, kupata maendeleo kwa muda mfupi kwa kuwa wananchi wake walikuwa nyuma kimaendeleo.

"Mimi ni shahidi hili Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, lilikuwa gumu mno na nyuma kimaendeleo kwa kuwa mama yangu Dk, Lucy Nkya, alishawahi kuwa Mmbunge wa jimbo hili na hakuna kijiji wala kata nisiyoijua au kufika, kweli Mbunge Babu Tale ameleta maendeleo," alisema Jonas.

> "Mimi ni shahidi hili Jimbo la Morogoro Kusini Masharikí, lilikuwa gumu mno na nyuma kimaendeleo kwa kuwa mama yangu Dk, Lucy Nkya, alishawahi kuwa Mmbunge wa jimbo hili na hakuna kijiji wala kata nisiyoijua au kufika, kweli Mbunge Babu Tale

Hata hivyo alitumia nafasi hiyo kuwataka wanachama wa CCM, kuachana na uhasama wa kisiasa ndani ya chama hicho, kwa kuwa wote wanajenga nyumba moja.

Akizindua maadhimisho hayo, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Josephat Masunga, ameonya watu walioanza harakati za kupita katika majimbo kabla ya kutangazwa kwa uchaguzi, akiagiza viongozi kuwa imara kwa ajili ya kuwabaini, ili wachukuliwe hatua ndani ya chama hicho.

# MAFANIKIO YA AFYA, MAJI, BANDARI NA ELIMU YATAJWA 'BIRTHDAY' YA DKT SAMIA



NA MWANDISHI WETU

MIKOA mbalimbali, taasisi, vikundi vya marafiki na wananchi mbalimbali juzi walishiriki kikamilifu kusherehea Siku ya kuzaliwa kwa Rais wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan, huku Mkoa wa Kagera ukiyataja mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana katika utawala wa Awamu ya Sita chini ya rais huyo hayapaswi kupita bila kupongezwa

Ukiacha shere za aina tofauti zilizofanyika katika Jiji la dar es salaam, lakini hata baadhi yao mikoa nayo imeripotiwa kufanya sherehe hizo za kumtakia maisha marefu na yenye afya kiongozi huyo wa nchi.

Kauli ya upendo nyingine imatokea mkoani Kagera kupitia Mkuu wake Fatma Mwassa ambaye alisema kuwa, Wakazi wa Mkoa Kagera kuwa hawana budi kumpongeza na kumuombea Sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan kutokana na shughuli nyingi za maendeleo zilizofanyika katika Mkoa huo. Akizungumza wakati wa sherehe za kumpongeza Mhe. Rais Dkt. Samia kwa kutimiza Miaka 65 ya kuzaliwa, zilizoandaliwa na Umoja wa Wanawake wa CCM Mkoa wa Kagera (UWT), Hajat Fatma Mwassa amesema mengi yanaonekana yaliyofanywa na Dkt. Samia yakiwemo yanayohusu Elimu, Afya, Barabara, Maji, Bandari, huku mengine yakiwa yamekamilika na mengine yakiwa katika hatua za kukamilika na mengine yakianzishwa.

"kwa uchache mmeona Vituo vya Afya na Hospitali zimejengwa ni Kazi ya Mhe. Rais Dkt Samia, mmeona Shule nzuri na Watoto wetu wanasoma vizuri ni kazi ya Dkt Samia, Mmeona Bandari zetu za Bukoba na Kemondo kila moja zimeletwa Shilingi Bilioni 22 kazi inakamilika kufikia Mwezi Machi, Barabara Njia Nne zinajengwa ni Kazi ya Dkt. Samia, Maji, Barabara, Umeme mpaka Vitongojini ni mengine mengi ni kazi ya Mhe. Rais Samia.." amesema Hajat Mwassa.

Aidha ameongeza kuwa ni muda sasa wa Akina Mama hao wa CCM kuendelea kukiimarisha Chama Cha Mapinduzi kwa kumpambania Rais Dkt. Samia kuhakikisha anapata Ushindi wa kishindo katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba Mwaka huu, kwa kumtafutia Kura hadi chini ya Uvungu, na kuzilinda kura hizo, ili kumpa nafasi ya Miaka Mitano mingine akamilishe Miradi mingine ya Maendeleo.

Sherehe hizo za kumpongeza Rais Dkt Samia zimefanyika Kata Kashai Bukoba Manispaa na Kuhudhuliwa na Viongozi pamoja na Wanawake wa UWT kutoka Wilaya zote za Mkoa Kagera.

# Nishati ya umeme yaifungua Bagamoyo

NA MWANDISHI WETU

VIJIJI na vitongoji kadhaa wilayani Bagamoyo mkoa wa Pwani vili vkuwa giza kutokana na kutopata nishati ya umme, vingine tangu ulipopatikana uhuru wa nchi hii mwaka 1961, lakini sasa maeneo mengi wanatos shukurani kwa Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuwezesha kuondoa changamoto hiyo.

Mfano ni Kijiji cha Saadan kilichokuwa katikati ya Hifadhi hiyo ambacho awali iliyogubikwa na giza, umasikini uliochagizwa ukosefu wa huduma za kijamii na kulifanya eneo hilo lisifikike kwa urahisiu kutokea katika miji mikubwa inayolizunguka kama vile yalipo makao makuu ya wilaya, Bagamoyo na Jiji la Dar es salaam.

Nyuma ya miaka ya 1960 hakukuwa na mwanga katika eneo hilo, wenyeji walioshi eneo hilo walijikita katika kazi ya uvuvi wakitumia nyenzo duni, pia kulikuwa na biashara nyingine kama vile ukataji wa ukindu, zao lililotumika sana kwa ajili ya ususi wa mikeka na vikapu, kadhalika ukataji miti ya Mikoko iliyokuwa ikisafirisahwa kwa majahazi kwenda katika miji ya Zanzibar na hata nje ya nchi Mombasa na Visiwa vya Comoro.

Mwanga ulijitokeza mwaka 1962 ilipoanzishwa Bustani ya wanyama, iliyojmumuisha wanyama wachache waliofungiwa katika Ng'enge (Zoo) kubwa na ndogo, zilizoanza kuvuta macho ya watalii kuanza kutembelea kijiji hicho kilichokuwa na wakazi wachache, wengi wao wakitokea maeneo mbalimbali ya nchi na kuafauata biashara ya uvuvi.

Enzi za Ukoloni Saadani iliwahi kukaliwa na Koloni la Waarabu walioendesha biashara ya utumwa, iliyotanabaishwa na kuwewpo mabaki ya magofu machache yaliyokuwa yakitumiwa katika biashara hiyo, pia gati kuu la kusafirishia watumwa kutoka bandari ndogo ya Saadani kuelekea Unguja na nchi nyingine za jirani.

Kwa mujibu wa simulizi za wazee wa mji huo hata jina hili la Saadani, lilitokana na Mzee mmoja wa Kiarabu aliyekuwa akimiliki saa ya ukutani, hivyo alipochoshwa na maswali ya kuulizwa muda "Saa ngapi? kila mara akawa anawajibu "kama unataka saa nenda kaangalie ndani.

Kwa vile hakuweza kutamka vizuri maneno ya Kiswahili ndipo alipokuwa akikatisha tu kwa kusema "Saadani" ndipo likazaliwa jina hili.

Ukuaji wa mbuga hiyo ya wanyama iliweza kuupa umaarufu mji huo mdogo ulipo kandoni mwa Bahari ya Hindi kwa kuanza kutembelewa na watalii pamoja na watu maarufu, akiwemo Mwanasiasa aliyeshika nyadhifa mbalimbali serikalini Mzee Rashid Mfaume Kawawa, aliyefika Saadani Mwaka 1974 na kuweka jiwe la Msingi la kumbukumbu ya ujiuo wake na uzinduzi wa bustani hiyo ya wanyama.

***Kufuatia kupatikana kwa nishati hiyo kijiji cha Saadan kilichokuwa kikikumbana na matukio ya kuvamiwa na wanyama wakati na waharibifu kama vile Tembo na Simba sasa imepungua na kuwa sehemu salama toka kijiji hadi mmbuga yenyewe.***

Kwa bahati nzuri kijiji cha saadan kiliweza kuonja maendeleo mapema kwa kupata zahanati pamoja na Shule ya Msingi iliyoanza ikiwa na madarasa manne na baadaye ikaendelea na kukamilisha madarasa yote saba, pia kiliwahi kununua gari aina ya Center kwa ajili ya shughuli za kijiji.

Kupitia uwepo wa bustani hiyi ya wanyama kijiji nhicho kilianza kupokea wafanyakazi wengi wakati huo wakijulikana kama 'Game Scout' kutoka maeneo mbali mbali na baadhi waliajiriwa wananchi wakazi wa kijiji hicho na vile vinavyozunguka bustani hiyo kama Uvinje, Buyuni Kuu na Buyuni Kitopeni.

Kwa kuwa mazingira ya hifadhi ya Saadani ni Jangwa wafanyabiashara wenye asili ya India chini ya Kampuni ya Albhai Panju and Sons walianzisha kilimo cha zao la chumvi na kuvuna maelfu ya tani waliyoisafisha kwenda maeneo mbalimbali ya nchi.

Kampunu hiyo iliweka kiwanda chake maeneo ya Malumbi nje kidogo ya Bustani ya Wanyama ya Saadan, na baadaye serikali kupitia Shirika la Madini la Taifa (Stamico) iliweza kuanzisha kiwanda cha kisasa cha uzalishaji chumvi na kupeleka watalaamu wa madini na kuanzisha mradi huo uliokuwa mkubwa sana.

Lakini katika kipindi chote Hifadhi hii iliyopo chini ya TANAPA, iliyoanzishwa mwaka 1962 ikiwa ni pori la akiba na Mwaka 2005, kupandishwa hadhi rasmi na kuwa hifadhi ya taifa, ikashuhudia ongezeko la wahamiaji waliovutwa na upatikanaji wa Samaki aina ya Kamba ambao katika kijiji hicho hujulikana kama Makaji ambayo yalikuwa yakiuzwa kwa bei kubwa na kuwa na maslahi mazuri kwa wavuvi.

Makampuni binafsi kama vile Dar Ocean Product na hata Tafico walikivamia kijiji hicho kwa ajili ya kununua samaki hao kutoka kwa wavuvi wenyewe moja kwa moja.

Lakini katika kipaindi chote hivyo huku zikipita awamu zote tano la utawala wa Serikali ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania wana kijiji walikuwa na changamoto mbalimbali za maendelo kama vile ukosefu wa nishati ya umeme na maji.

Kadhalika miundombinu ya barabara inayotokea mwishoni mwa daraja la kisasa la Wami kuingia kulia katika Vijiji vya Mandela na baadaye Miono, Zimbili, Mkange na kuingia Saadan ilikiuwa ipo katika hali mbaya.

Serikali ikaifanyia kazi changamoto hiyo baada ya kufanya ujenzi wa kisasa wa baraba inayotokea eneo la Makurunge Bagamoyo yalipokuwa mashamba ya mifugo ya Ranchi ya Zanzibar Bagamoyo (RAZABA) hadi kuingia Kijiji cha Saadani kupitia miji iliyokuwa kandoni mwa bahari ya Hindi kama vile Mkwaja na Buyuni.

Katika utawala huu wa awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan, Mbunga ya Saadani inang'aa,baada ya kupatiwa umeme wa kutosha.

Kwa takriban mwaka sasa wakazi wa Saadani wanafaidika na uwepo wa nishati ya umeme, waliyoikosa tangu nchi kupata uhuru.

Kufuatia kupatikana kwa nishati hiyo kijiji cha Saadan kilichokuwa kikikumbana na matukio ya kuvamiwa na wanyama wakati na waharibifu kama vile Tembo na Simba sasa imepungua na kuwa sehemu salama toka kijiji hadi mmbuga yenyewe.


Hivi sasa mkazi wa Saadani atakayetafuta bughudha ya kukutana na wanyama ni yule atayekwenda misituni kwa ajili ya kufanya shuguli za kibinadamu kama vile kuzoa chumvi au kuvua katika maeno yasiyokuwa rasmi kwa shuguli hiyo.

Wakazi wa Saadani kwa sasa wanaliimba jina la Rais Samia kwamba ndiye aliyendika historia ya kuing'arisha Saadani, kizazi kipya kutoka eneo hili sasa hakina tena histoiria ya enzi hizo ambazo wakazi walifuata taa aina ya Karabai iliyokuwa ikiwashwa na wafanyabiashara maarufu enzi hizo Mohamed Mwarabu al maarufu Mzee Ganda na Mfaume Akida Mimi na Sheikh Said waliokuwa wakimiliki maduka zama hizo.



# TRUMP AENDELEA KUINYIMA USINGIZI URUSI

NA MWANDISHI WETU



KUREJEA madarakani kwa Donald Trump, ambaye hapo awali aliahidi kumaliza vita nchini Ukraine, kumeibua hali mpya ya wasiwasi miongoni mwa makampuni ya Magharibi ambayo bado yanaendelea kufanya shughuli zake nchini Urusi.

Hali hii inatokea wakati serikali ya Urusi ikiendelea kuimarisha sheria na masharti yanayoongeza gharama za kujiondoa kwenye soko lake, pamoja na kutoa vivutio finyu kwa wanaotaka kuendelea kufanya biashara nchini humo.

Tangu Moscow ilipoivamia Ukraine mnamo Februari 2022, makampuni makubwa kama Renault, McDonald's na Heineken yaliondoka Urusi, yakiuza hisa na mali zao kwa hasara kubwa kufuatia sheria kali zilizowekwa.

Baadhi ya makampuni mengine, hususan yale ya vyakula na bidhaa za usafi kama PepsiCo, Procter & Gamble na Mondelez, bado yanaendelea kufanya shughuli zake nchini Urusi kwa kile wanachokiita "sababu za kibinadamu."

Benki kadhaa za Ulaya kama Raiffeisen Bank International na UniCredit nazo zinajikuta katika mtanziko huohuo, zikikabiliwa na ugumu wa kurejesha mali zao zilizozuiliwa nchini Urusi.

Tayari, serikali ya Moscow inadai punguzo la angalau asilimia 60 wakati wa miamala ya kuondoka, sambamba na 'mchango wa hiari' wa asilimia 35 kwenye bajeti yake, ambao Marekani imeuita "kodi ya kuondoka."

Je, Trump atafanya nini?

Wadau mbalimbali wa kibiashara na kisheria, akiwemo Ian Massey, mtaalam wa biashara, wanasema ushindi wa Trump unaongeza sintofahamu kwa mashirika yenye mali au vitegauchumi nchini Urusi.

Kremlin inatarajiwa kuendelea kuongeza gharama za kujiondoa ili kufidia hasara, huku Trump akitabiriwa kupunguza gharama za uendeshaji kwa makampuni yanayopendelea kuwekeza au kurejea Marekani.

"Inatarajiwa itachukua miezi kadhaa kuumaliza mzozo wa Urusi na Ukraine, hata kama Trump ataingilia kati," anasema Massey. "Hivyo, makampuni yatakuwa yakitathmini mikakati yao kwa umakini zaidi."

Baadhi ya wachambuzi wanaamini kurejea kwa Trump kunaweza kuwapa uwezekano mpya makampuni yanayotaka kuendelea na biashara zao Urusi, ikiwa vikwazo vya kimataifa vitaregezwa. Kwa upande mwingine, huenda yakatokea mazingira yatakayoharakisha makampuni mengine kukamilisha mpango wao wa kujiondoa kabisa.

Sheria za Moscow zinavyozidi kuwa kali

Kwa mujibu wa Alexei Yakovlev, mkurugenzi katika Wizara ya Fedha ya Urusi, mazungumzo ya mikataba ya kuondoka kwa makampuni fulani bado yanaendelea.

Hata hivyo, hakufafanua ikiwa kurejea kwa Trump kunaweza kuzuia hatua za makampuni hayo au kusaidia mengine kurejea nchini Urusi.

Serikali ya Urusi imesisitiza kuwa mpango wowote wa kujiondoa unaohusisha dola milioni 488 au zaidi, lazima upitishwe na Rais Vladimir Putin.

Aidha, wanunuzi wa ndani wanaotaka kununua mali za makampuni ya nje, wanapaswa kuonyesha mkakati mahsusi, likiwemo jinsi gani kununua au kutonunua biashara husika kunavyoweza kuathiri uchumi wa Urusi.

Mustakabali uliojaa sintofahamu

Mengi yamebadilika tangu mwaka 2022, wakati makampuni mengi yalianzisha mazungumzo ya kujiondoa. Kwa sasa, mchakato huo ni mgumu zaidi kutokana na:

Tathmini ya Thamani: Thamani ya makampuni inahitajika kuthibitishwa na wataalam huru wanaoteuliwa na Wizara ya Uchumi ya Urusi.

Minada ya Uwazi: Serikali inaendesha minada ili kuwapa wanunuzi wote wa ndani fursa sawa, jambo linalowapa makampuni ya Magharibi hofu ya kushindwa kupata bei nzuri.

Kurejea kwa Trump madarakani kumebadili kabisa ramani ya kisiasa na kiuchumi, na huenda kukabadilisha mwelekeo wa makampuni ya Magharibi yanayoyumba kati ya kuondoka au kuendelea kubaki Urusi.

Hata hivyo, mwelekeo huu unatabiriwa kuambatana na mifumo mipya ya kisheria inayodhibiti mtiririko wa rasilimali na fedha.

Bado hakuna uhakika juu ya lini vita vya Ukraine vitakoma, au jinsi Trump atakavyoshughulikia mgogoro huo na vikwazo dhidi ya Urusi.

Wakati uamuzi wa mwisho ukisubiriwa, makampuni ya Magharibi yanajikuta kwenye maamuzi magumu zaidi kuliko wakati wowote ule.

Je, yatadumu Urusi, kuondoka sasa, au kusubiri kuona iwapo sera za Trump zitapunguza gharama zao za uendeshaji na athari za vikwazo?

Ni wazi kuwa mustakabali wa uchumi wa kimataifa unazidi kugubikwa na hali ya kutokuwa na uhakika, huku macho ya wachumi na wafanyabiashara wengi yakielekezwa kwenye Ikulu ya Marekani na Kremlin.



# Michezo Kimataifa

## Tetesi za soka




MANCHESTER United wameomba kufahamishwa kuhusu mustakabali wa mshambuliaji wa Chelsea na Ufaransa Christopher Nkunku, 27, huku winga wa Argentina Alejandro Garnacho, 20, akihusishwa na uhamisho wa kwingineko.



JUVENTUS wameipa Chelsea ruksa ya kumsajili kiungo wa kati wa Brazil Douglas Luiz, 26, ambaye pia ananyatiwa na Manchester City na Arsenal, hii imetokana na mazungumzo mazuri kati ya klabu hizo na pia maslahi yaliyoridhiwa na pande hizi mbili.




1

MANCHESTER United huenda ikamsajili mshambuliaji wa Chelsea na Ufaransa Christopher Nkunku, 27, kwa mkopo ikiwa Muingereza Marcus Rashford, 27, ataondoka katika klabu hiyo. (The Athletic – Usajili unahitajika)

BAADA ya kulaulimiwa kwa muda mrefu kuwa tatizo la Arsenal ni kudharau kufaya usajili hasa eneo la ufungaji, hatimaye klabu hiyo imesikia kilio hicho na sasa imeanza mawindo makali ili kutibu pengo lililopo, kufutia mkakati huyo klabu hiyo imeingia chimbo na kumnasa Straika makali Raia Slovenia anayekipiga katika klabu ya RB Leipzig ya Ujerumani





## RASHFORD ANAVYOPASUA VICHWA VYA FAMILIA YA SOKA

NA MWANDISHI WETU

KOCHA wa Manchester United, Ruben Amorim amegonga vichwa vya habari aliposema, ni bora kumuweka kama mchezaji wa akiba kocha wake wa makipa mwenye umri wa miaka 63, kuliko Marcus Rashford, kwa sababu hana juhudi.

Rashford hajacheza kwenye kikosi cha United kwa muda wa wiki sita. Amorim anasema mshambuliaji huyo wa Uingereza hafanyi vyema katika mazoezi.

Mustakabali wake ndani ya Old Trafford haujulikani. Kuna klabu za Ulaya zinazohusishwa na kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, kabla ya tarehe ya mwisho ya uhamisho wa wachezaji wiki ijayo.

Sio mara ya kwanza kwa kocha wa Ligi Kuu England kumkosoa hadharani mmoja wa wachezaji wake.

Harry Redknapp na Darren Bent Harry Redknapp alidai kuwa mke wake angefunga, pale Darren Bent alipokosa bao dakika za lala salama. Siku Tottenham ilipotoka sare ya 1-1 na Portsmouth Januari 2009.

Redknapp alisema: “Huwezi kupata nafasi nzuri zaidi ya kushinda goli kuliko ile uliyoipata. Hata mke wangu angeweza kufunga.”

Licha ya kauli hiyo, Bent alibaki kwenye safu ya wachezaji wa Redknapp na alimaliza msimu wa 2008-09 kama mfungaji bora wa Tottenham akiwa na mabao 17, kabla ya kujiunga na Sunderland majira ya kiangazi.

Redknapp alitumia miaka mingine mitatu na nusu akiwa White Hart Lane (Tottenham) akiwasaidia kufika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa mwaka 2011, lakini alitimuliwa Juni 2012.

Harry Redknapp na Adel Taarabt Redknapp, wakati huo akiwa meneja wa QPR, hakusita kumkosoa Adel Taarabt alipoulizwa kwa nini kiungo huyo ameachwa nje ya kikosi kwenye mchezo dhidi ya Liverpool,

# Burudani



## Msondo Ngoma wamwimbia Dkt Samia

NA MWANDISHI WETU

BENDI kongwe ya muziki wa dansi Msondo Ngoma wiki hii imemaliza mazoezi ya wimbo maalum waliouandaa kwa ajili ya kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan, wimbo huo ambao umeanza kupingwa katika maeneo mbalimbali inapofanya maonyesho yake ya wiki, umeanza kuwa kivutio kwa mashabiki.

Akizungumza na gazeti hili Meneja wa bendi hiyo Saidi Kibiriti alisema, hao kama Tasisi wameona juhudi za makusudi zinazofanywa na kiongozi huyo na kuona ipo sababu ya kumpa maua yake.

Naye mkuu wa Jukwaa wa bendi hiyo Juma Katundu alisema kuwa katika wimbo huo wanazungumzia baadhi ya manufaa waliyopata Watanzania katika kipindi cha Utawala wa awamu ya sita kama vile ujenzi wa reli ya kisasa pamoja na usafiri wa Treni ya umeme, pia miundombinu na ukuaji wa uchumi mambo ambayo kwa sasa yanaonekana hata kwa macho.

Alisema wimbo huo utakapokamilika watarekodi na kisha kuusambaza katika vituo vya redio na Televisheni ili Watanzania waone kazi hiyo iliyolenga kutoa wasifu na kuzitambua juhudi zinazofamnywa na viongozi katika mikakati ya kuendeleza taifa la Tanzania.

Alisema huo ni mwanzo lakini bendi hiyo itakuwa ikitunga nyimbo kama hizo kwa ajili nya viongozi mbalimbali na hata watu wengine wanaojitolea kusaidia masuala ya kijamii katika nchi hii.

## Jb atamani waigizaji wapya

NA ERYNE BANDA

MSANII mkongwe wa Bongo Movie, Jacob Steven 'JB', amesema sababu za maprojuza kurudia wasanii wale wale kwenye filamu na tamthilia ni kutokana na uwepo wa waigizaji wachache wenye uwezo huo.

JB alisema atamani wapate waigizaji wapya wenye uwezo mkubwa zaidi, ndiyo maana yuko bize kufanya usaili wa waigizi wapya ili kuleta sura mpya kwenye uigizaji kwani mashabiki wamechoka kuona waigizaji ni wale wale hawabadiliki.

"Mashabiki wasitulaumu sana kwa maprojuza kurudia wasanii wale wale kwenye filamu na tamthilia. Sababu ni tasnia ya uigizaji ina waigizaji wachache wenye uwezo wa kuigiza. Ndiyo sababu mashabiki wanaona hawabadiliki.

Binafsi nimeligundua hilo na natamani nipate waigizaji wapya wenye uwezo mkubwa zaidi, ndiyo maana niko bize sasa hivi kufanya usaili wa waigizi wapya ili kuleta sura mpya kwenye uigizaji," alisema JB.





## Belle 9 ammwagia sifa Ben Pol

NA EMMANUEL TAIRO

STAA wa RnB Bongo, Abednego Damian 'Belle 9', ameweka wazi kuwa, katika utaratibu wake wa kufanya kazi haangalii wala kuchagua wa kufanya naye.

Belle 9 ambaye aliwahi kutamba na ngoma ya 'Sumu ya Mapenzi "Najua watu huwa tunasahau fadhila na mimi kiukweli nisiwe mchoyo wa kutoa shukurani, ninamshukuru sana, Ben Pol kwa mambo aliyoweza kunifanyia mpaka hapa nilipofikia.

"Alikuwa mwalimu mzuri sana kwangu na alikuwa anapenda nitimize ndoto zangu, hakutaka nikate tamaa kabisa," anasema Belle 9

Mwimbaji huyo ameliambia Gazeti la Jamvi la Habari kuwa, msanii anayejiamini kwenye kazi zake haoni sababu ya kuanza kuchagua watu wa kufanya nao kazi, bali kuona wasanii wachanga wanafika mbali.

## Mlela: Sanaa inatakiwa ikue

NA EMMANUEL TAIRO

MKALI katika tasnia za filamu, Yusuf Mlela amesema kutokana na mabadiliko yanayohitajika kwenye sanaa, haoni tatizo wasanii wa Bongo Fleva wakiingiza kwenye filamu na tamthiliya.

Akizunguza na mwandishi wa gazeti hili, Mlela ambaye ukiachilia mbali na uigizaji pia ni muongozaji wa tamthilia, amesema kuwa sanaa kila siku inatakiwa ikue ndiyo maana wasanii wengi wa Bongo Fleva wameamua kufanya hivyo.

"Unajua sanaa inatakiwa ikue kila siku mambo yanatakiwa mapya, ukiangalia sisi wote ni wasanii na msanii lazima aweze kuonyesha uwezo wake katika sanaa, acha waingie ili kuleta vitu vya tofauti," alisema Mlela.

JAMVI LA HABARI
SPOTI
IJUMAA JANUARI 31, 2025




## Mbosso akaa kimya tetesi kusepa WCB

>> Soma Uk. 15

# KEN GOLD YAKUSANYA WAKONGWE SIMBA, YANGA



NA MWANDISHI WETU

TIMU ya Ken Gold ya Jijini Mbeya inayoshiriki Ligi Kuu NBC, imeanika usajili wake iliyoufanya katika usajili wa dirisha dogo, huku sura za wachezaji waliowahi kuzichezea klabu kongwe za Simba na Yanga zikitawala.

Lengo la timu hiyo iliyopanda daraja msimu uliopita ni kuimarisha kikosi chake ili iweze kujinusuru katika janga la kushuka daraja, kutokana na matokeo mabaya iliyoiyapata tangu ilipoanza michuano hiyo ambayo sasa inaelekea mzunguko wa pili.

Ken Gold inaburuza mkia katika msimamo wa ligi hiyo baada ya kucheza michezo 16 lakini ikiambuilia ponti sita tu na kuendelea kuzibeba timu nyingine 15 juu yake.

Wachezaji waliotajwa kusajiliwa katika kipindi hiki ambao tayari wameshaanza kuonekana uwanjani ni pamoja na beki wa kati Zawadi Mauya na Benard Morrison waliowahi kukipiga katika kikosi cha Yanga, pamoja na Obrey Chirwa ambaye naye alipoita kwa Wanajangwani hao na kisha kuchezea timu mbali mbali na sasa ametua katika kikosi hicho.

Mkongwe mwingine ambaye usajili wake umezusha minong'ono ni Kelvin Yondan mwenye umri wa miaka 40 ambaye kwa kipindi cha muda mrefu hakuonekana uwanjani baada ya timu yake Geita Gold kushuka daraja na sasa amaibukia katika kikosi hicho.

# Yanga macho yote kwa Ikangalabo

NA MWANDISHI WETU

NI kama vile mashabiki wa klabu ya Yanga hawajapata muda mzuri ya kumuangalia na kumfanyia tathmini winga wao mpya Jonathan Ikangalabo, aliyesajiliwa katika kipindi cha dirisha dogo, hivyo wanatamani Jumamosi ifike hata leo ili waweze kumuona nyota wao huyo.

Yanga itaumana na Kagera Sugar katika mchezo wa Ligi Kuu ya NBC Jumamosi katika uwanja wa KMC, ambapo taarifa zinadokeza kuwa kocha Mkuu wa Yanga Sead Ramovic amepanga kutumia mchezo huo kumjaribu Ikangabo aliyesajiliwa kutoka As Vita ya nchini DRC.



Kabla hajajiunga na Yanga winga huyo alikuwa tegemeo akiisaidia sana timu hiyo ya awali ambapo Yanga ilivutika naye baada ya kuona kiwango chake.

Inadaiwa Ikangalabo licha ya kucheza nafasi zote za pembeni lakini ni mchezaji mwenye kasi kubwa na uwezo wa kupachika mabao kutokea pembeni, pia ni mtaalamu wa kujpiga kona.



## RATIBA YA LIGI KUU BARA BONGO HII HAPA

**BURUDANI** ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inadhaminiwa na NBC inarejea kwa mara nyingine tena baada ya muda kidogo kusimama kutokana na ratiba ya Mapinduzi Cup na Fainali za Mataifa ya Afrika.

>> Inaendelea Uk. 14